

102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
LUGHA
JULAI/AGOSTI 2010
MUDA: SAA 2 ½

TATHMINI YA PAMOJA YA WILAYA ZA BORABU-MASABA – 2010
Kenya Certificate of Secondary Education – (KCSE)

KISWAHILI
KARATASI YA 3
LUGHA
JULAI/AGOSTI 2010
MUDA: SAA 2 ½

Maagizo

- a) Jibu maswali manne pekee.
- b) Swali la kwanza ni la lazima.
- c) Chagua mengine matatu kutoka sehemu nne zilizobaki yaani: Riwaya, Tamthilia, Hadithi Fupi na Ushairi.
- d) Usijibu maswali mawili kutoka katika sehemu moja.
- e) Majibu yaandikwe katika kijitabu cha majibu utakachopewa.
- f) Hakikisha kuwa kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kwamba maswali yote yamo.

*Karatasi hii ina kurasa nne zilizopigwa chapa.
Mtahiniwa ahakikishe kwamba kurasa zote zimepigwa chapa sana sana na kuwa maswali yote yamo.*

1. (LAZIMA) FASIHI SIMULIZI

- a) Nini maana ya maghani? (alama 2)
- b) Eleza sifa zozote sita za maghani. (alama 6)
- c) Dhihirisha tofauti ya kimsingi iliyopo baina ya maghani ya kawaida na yale ya masimulizi. (alama 4)
- d) Taja na ueleze kwa ufupi vipera vyovyote vitatu vya maghani ya kawaida. (alama 6)
- e) Pendekeza hoja mbili kuonyesha dhima ya maghani katika jamii. (alama 2)

RIWAYA

Utengano: S. A Mohamed

Jibu swali la 2 au 3.

2. “Alikuwa akimaliza kilio chake cha ghadhabu alichokuwa akilia miaka kwa miaka. Lakini hatimaye alinyamaza na kilio chake kilikatika moja kwa moja na chozi lake, lile aliloliita, ‘chozi la mliwa’ lilikauka moja kwa moja pia.”
- a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
- b) Tambua sifa za mrejelewa kulingana na jinsi alivyosawiriwa riwayani. (alama 4)
- c) Onyesha ni kwa nini chozi la mrejelewa linaitwa la ‘mliwa’. (alama 6)
- d) Kwa kurejelea riwaya ya utengano, taja wahusika wengine watatu wa jinsia ya mrejelewa waliolia kwa ‘kuliwa’ na ueleze jinsi ‘walivyoliwa’. (alama 6)
3. ‘Hulka ya wahusika hubadili mikondo kila uchao’. Fafanua kwa kudondoa mifano mwafaka katika riwaya ya utengano. (alama 20)

TAMTHILIA

Kifo Kisimani: Kithaka wa Mberia

Jibu swali la 4 au 5.

4. “Yetu imekuwa na vikwazo kwa miongo miwili..... ukitaka nikuitie silaha yako nitakuitia...”
- a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
- b) Taja mbinu moja ya lugha iliyotumiwa kufanikisha ujumbe wa mwandishi katika dondoo hili na uitolee mifano miwili. (alama 3)
- c) Fafanua ‘vikwazo’ anavyorejelea mzungumzaji. (alama 7)
- d) Wanaharakati wa Butangi walitumia mbinu mbalimbali katika juhudi yao ya kuondoa ‘vikwazo’ vinavyorejelewa. Thibitisha. (alama 6)

5. Vijana na wanawake wanaweza kutekeleza majukumu muhimu katika jamii. Fafanua ukirejelea tamthilia ya Kifo Kisimani. (alama 20)

HADITHI FUPI.

Mayai waziri wa maradhi na Hadithi Nyingine: K.W. Wamitila

6. Matukio mengi katika Diwani ya Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine yanaenda na wakati. Thibitisha. (alama 20)

USHAIRI

7. Soma shairi lifuatalo halafu ujibu maswali.
NIMO: Mahiri Mwita.

Nimo ndimo mi nilimo, simo simostahili,
Nimo niwajibikamo, simo mwenye ujahili,
Nimo nikusudiamo, simo wanamodhalili,
Nimo na nitakikamo, simo nami kwa thakili,
Nimo kwa kina na kimo, simo kwa wasiobali,
Nilimo ndimo.

Nimo nimuchunguamo, simo mnamodekezwa,
Nimo nimufikirimo, simo nilimodumazwa,
Nimo haki munyimwamo, simo mnamotukuzwa,
Nimo namo msimamo, simo mnotumbuizwa,
Nimo nayo yaliwamo, simo mwa kuteterezwa,
Nilimo ndimo.

Nimo kisa cha kuwamo, simo nilimolimbikwa,
Nimo nitakase mumo, simo ilikuzugikwa,
Nimo kwani waliomo, simo bali wametekwa,
Nimo walifungiwamo, simo, kwani wamezikwa?
Nimo uhai uwemo, simo mwa waliozikwa,
Nilimo ndimo.

Nimo waja waliomo, simo wanamomutaka,
Nimo walizawamo, simo, kwayo takataka,
Nimo nimulike mumo, simo ili kuposeka,
Nimo nitie kikomo, simo, nafuu talaka,
Nimo bali sitawemo, simo kuacha mabaka,
Nilimo ndimo.

Nimo nitawana mumo, simo musimodhikika,
Nimo hadi na kikomo, simo nitamoridhika,
Nimo nawe uliyemo, simo kunafsikika,
Nimo mbona nisiwemo, simo kuvikwa ukoka,
Nimo na wenye midomo, simo humo kupayuka,
Nilimo ndimo.

- a) Taja bahari mbili zilizozingatiwa kutunga shairi hili na utoe sababu kwa kila jibu lako. (alama 2)
- b) Kwa nini mtunzi akatumia neno ‘nikusudiamo’ badala ya ‘ninamokusudia’ katika ubeti wa kwanza? (alama 4)
- c) Eleza mambo yoyote manne yanayomkera msanii katika shairi. (alama 4)
- d) Andika ubeti wa nne kwa njia ya nathari. (alama 4)
- e) Onyesha tamathali mbili za semi zilizotumiwa kuendeleza ujumbe shairini. (alama 2)
- f) Fafanua umbo la shairi hili. (alama 4)
- g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kulingana na jinsi yalivyotumika shairini.
- i) Wanamodhalili
 - ii) Wasiobali